

Mboga ya majani ya kisamvu ni chanzo cha vitamin vihitajikavyo na mwili wa binadamu. Ingawa mboga za mbichi za majani zina vitamin vya kutosha lakini upatikanaji wake huwa ni wa msimu. Ili mkulima/kaya iwe na uhakika wa kupata mboga za majani wakati wote ni muhimu watumiaji wafahamu teknolojia bora za utayarishaji na uhifadhi wa mboga hizo. Ni vigumu kuhifadhi mboga mbichi na hudumu kwa muda mfupi sana kutokana na uharibifu unaosababishwa na vimelea vya wadudu na magonjwa.

Lengo la mafunzo yetu ni kumwezesha mkulima/kaya kuweza kuhifadhi mboga ya majani ya kisamvu wakati wote na kuelewa teknolojia ya matumizi ya **solar drier** katika kukausha mboga. Makala hii itaanisha hatua kwa hatua katika kufikia upatikanaji wa mboga bora.

**Mambo ya kuzingatia wakati wa kukausha mboga**

Usafi wa mkaushaji mboga
Mboga zivunwe mara moja, kuchambuliwa na kuoshwa kwa kutumia maji safi na salama.
Eneo la kufanyia kazi liwe safi
Visu viwe visafi

**Utayarishaji wa 5i)-4(k)11(a k)9(uf)-3(i)-4(k)11a 1 108 0 F 11.0f1 0 0 1 hizo. N-**

Mahali safi au kabati la kuhifadhia



**Namna ya kutambua mboga zilizokausha vizuri**

Ukifikicha katika kiganja ungauunga hutoka kwa urahisi
Mboga huwa nyepesi na hutoa harufu nzuri.

**Ufungashaji wa majani ya kisambu yaliyokaushwa**

Wataalamu wanashauri ufungashaji wa kisamvu kilichokauka ufanyike wakati wa mchana kwenye hali ya jua kali ambapo unyevu unakuwa mdogo ili kuzuia mboga kunyonya unyevu na kuleta uharibifu wa haraka. Ni muhimu mboga ifungashwe kwenye mifuko ya nailoni ambayo haipitishi maji.

**Uhifadhi wa majani ya kisamvu yaliyokaushwa.**

Mboga zilizokaushwa zihifadhiwe mahali pakavu, penye ubaridi na pasipofika panya. Ni vizuri kuhifadhi majani ya kisamvu yasiyosagwa hadi wakati wa kutumika kwani mboga iliyosagwa huharibika mapema. Majani ya kisamvu yaliyokaushwa na kuhifadhiwa vizuri huweza kukaa kwa mwaka mmoja.

**Kudhiti ubora wa bidhaa**

Chagua majani ya kisamvu yaliyotayari kuvunwa ambayo ni laini yasiyo makavu
Chambua mboga na ondoa majani yasiyofaa
Tumia maji safi katika kuosha mboga
Katakata mboga kwa ukubwa unaolinga
Weka mboga katika mifuko ya nguo na chovya kwenye maji yanayochemka. Maji yawekwe chunvi kidogo.
Acha mboga ipoe na uweke kwenye kaushio (solar drier). Hakikisha mboga haijazwi kupita uwezo wake.
Kagua joto la kaushio (solar drier) lisizidi nyuzi joto 60 za sentigredi.
Hakikisha unafungasha mboga katika uzito sawa kama ilivyoainishwa kwenye lebo
Tumia lebo inayokubalika kisheria
Hifadhi mboga mahali safi, pakavu, penye baridi na pasipo na mwanga mkali.

**9) Draft budget for the training program -- prepare this page as if it were part of a proposal that you**

**wish to get funded**

**Proposed budget for Training - EXCHANGE RATE: 1 USD = Tzshs1600**

| ITEM | Budget notes | TZSHS | USD |
|---|---|---|---|
| 1.0 Preparation of training material and translation | Fee for 2 trainers each 30,000 Tshs x 2 days | 120,000 | 75 |

1.1 Training fee for 2 trainers